

Maswali

1. Nani hakupenda marafiki wa Yesu?
2. Sauli alifanya nini kwa wote waliofundisha juu ya Yesu?
3. Sauli alienda wapi tena kuua marafiki wa Yesu?
4. Sauli aliona nini njiani?
5. Sauti iliambia Sauli nini?
6. Nini ilifanyika Sauli alipoamka na kufungua macho yake?
7. Yesu aliambia Sauli aende wapi?
8. Yesu aliambia nani aende kumsaidia Sauli apate kuone?
9. Mbona Anania hakutaka kwenda kumsaidia Sauli?
10. Yesu aliambia Anania eti nini?
11. Sauli alifanya nini wakati Anania alipomponya macho yake?

Majibu

1. Sauli hakupenda marafiki wa Yesu.
2. Sauli aliwaweka gerezani.
3. Sauli alienda Dameski.
4. Sauli aliona mwangaza kuu.
5. Sauti iliuliza Sauli, “Mbona haunipendi mimi na marafiki wangu?”
Sauli aliuliza, “Wewe ni nani Bwana?” Sauti ilimjibu, “Mimi ni Yesu.”
6. Sauli alikuwa kipofu.
7. Yesu aliambia Sauli aende aishi kwa Njia Nyofu iliyoko Dameski.
8. Mungu alimwambia Anania aende afungue macho ya Sauli.
9. Kwa sababu alijua kwamba Sauli alikuwa amekuja kuwakamata marafiki wa Yesu
10. Aliambia Anania kwamba Sauli alikuwa amechaguliwa kufundisha juu ya Yesu.
11. Sauli alisikitika kwamba alikuwa amewaweka marafiki wa Yesu gerezani. Alibatizwa. Alianza kufundisha juu ya Yesu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



49 Sauli anakuwa Mkristo

Marejeo

Matendo ya Mitume 9: 1 – 22

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alimchagua Sauli ahubiri injili. Sauli alipoamini katika Yesu alibadilisha maisha yake kabisa.

Maneno maalum


- 49.1 Sauli + chukia + marafiki wa Yesu + Kuhani Mkuu + barua + gereza + Dameski +
- 49.2 Sauli + wanaume + Dameski + mwangaza kuu + sauti + mbona unanichukia? + u nani? +Mimi ni Yesu
- 49.3 Sauli + kipofu + Dameski + Njia Nyofu + Anania + Yesu + enda kwa Sauli + hakutaka kwenda + Sauli amechaguliwa + Anania alienda
- 49.4 Anania + guza + macho ya Sauli + magambi + ona tena +Sauli aliamini + sikitika + batizwa + funza juu ya Yesu.

49.1 Sauli alichukia watu wote waliopenda Yesu. Aliudhika kwa sababu waliambia kila mtu juu ya Yesu. Sauli hakuamini kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Alitaka kuzuia wanafunzi na marafiki wa Yesu wasizungumze juu ya Yesu. Sauli alienda kwa Kuhani Mkuu. Alipewa barua ya kusema kwamba ameruhusiwa kukamata na kuweka gerezani mtu yeyote aliyefundisha juu Yesu.

Watu wengi wa Yerusalemu walifundisha juu ya Yesu. Sauli aliweka wengi sana kwa gereza. Lakini Sauli alikuwa bado na hasira. Baadhi ya marafiki wengi wa Yesu walikuwa wamesafiri mpa kwa mji wa Dameski. Walikuwa wako wanafundisha watu juu ya Yesu na vile amefufuka kutoka kwa wafu. Kwa hivyo Sauli aliuliza Kuhani Mkuu ampe barua ingine. Barua ilisema kwamba anaweza kumkamata mtu yeyote huko Dameski aliyefundisha juu ya Yesu. Angewarudisha Yerusalemu kuwekwa kwa gereza.

49.2 Sauli alichukua watu wengine na wakaanza safari ya kwenda Dameski. Safari hiyo iliwachukua siku kadha. Mwishowe waliweza kuona huo mji wa Dameski kwa umbali. Kwa ghafula kulitokea mwangaza mwingi, mwingi kuliko jua uliomulika kutoka angani na ukazunguka Sauli. Sauli alianguka chini na akasikia sauti ikisema, “Sauli, Sauli mbona unanichukia mimi na marafiki zangu?”

Sauli aliuliza, “Wewe ni nani, Bwana?” Sauti ilimjibu, “Mimi ni Yesu. Unawaweka marafiki wangu gerezani. Euka na uende mjini, kule utaambiwa chenye lazima ufanye kule.”



49.3 Sauli aliinuka pole pole. Alipofungua macho yake, hangeona kitu. Alikuwa kipofu. Kwa hivyo aliongozwa na watu mpaka Dameski. Sauli aliishi Njia Nyofu kwa mtu aliyeitwa Yuda.

Dameski, aliishi rafiki wa Yesu jina lake Anania. Yesu alizungumza naye kwa ndoto, “Anania, enda kwa Njia Nyofu. Kule utapata mtu jina lake Sauli, anaishi kwa nyumba ya Yuda. Yeye ni kipofu. Lazima umsaidie apate kuona tena.” Anania hakutaka kwenda. Alijua kwamba Sauli alikuwa anakuja kukamata marafiki wa Yesu. Yesu alimwambia kwamba Sauli alikuwa amechaguliwa kwenda kufundisha mataifa juu yake. Halafu Anania akaenda.

49.4 Anania alienda na akamkuta Sauli. Aliguza macho za Sauli na vitu kama magambi zikaanguka chini. Halafu Sauli akaanza kuona. Sauli alishukuru Mungu na Anania kwa kumsaidia apate kuona tena. Sauli alijua kwamba amekuwa na makosa sana. Aliamini kwamba Yesu yu hai tena. Alijua ni lazima ambie watu juu ya Yesu. Alisikitika sana kwa sababu alikuwa ameweka maarafiki wa Yesu gerezani. Kwa hivyo Sauli alibatizwa kuonyesha kwamba anasikitika. Aliahidi kwamba atajaribu kuishi akimtumikia Mungu na Yesu. Yesu alisamehe Sauli kwa kuweka marafiki wake kwa gereza. Sauli alitumia muda wake na maisha yake kufundisha watu juu ya Yesu.

